



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UDHIBITI WA USALAMA KWA MADEREVA NA WAMILIKI WA VYOMBO VYA MOTO KIBIASHARA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani na wadau wengine, tunaendelea kutekeleza jukumu la kusimamia usalama wa huduma za usafiri kwa magari ya abiria na mizigo nchini kwa mujibu wa Sheria.

Miongoni mwa majukumu yanayotekelawa na LATRA kwa lengo la kuimarisha usalama ni kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa. Tarehe 22 Februari, 2023, kwenye kikao cha wadau wa usafirishaji, Mhe. Eng. Hamad Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alitangaza kuwa madereva wote wa vyombo vya moto kibiashara wahakikishe wamesajiliwa LATRA kabla ya tarehe 30 Aprili, 2023. LATRA imeendelea kuwasajili madereva wa vyombo vya moto kibiashara na inawashukuru madereva ambao wamejitokeza kwa wingi ili kusajiliwa kwa lengo la kuthibitishwa.

Hata hivyo, zoezi la usajili wa madereva limekuwa na changamoto ambazo zimesababisha kutekelezwa kwa kasi ndogo na hivyo kutofikia malengo. Changamoto zilizobainika wakati wa usajili ni pamoja na ugumu wa kupata vyeti vya kuthibitishwa afya kwa madereva na ukosefu wa vyeti vya mafunzo ya udereva. Ili kupunguza changamoto hizo, LATRA imechukua hatua ya kuongeza muda wa madereva kusajiliwa hadi tarehe 31 Julai, 2023 na kuondoa kwa muda hitaji la madereva kuwa na cheti cha kupima afya.

Kipindi hiki cha miezi mitatu, kitatoa nafasi kwa madereva walioshindwa kusajiliwa kwa kukosa vyeti vya mafunzo ya udereva, kuhudhuria mafunzo hayo. Tunawapongeza madereva na waongoza watalii zaidi ya 500 wa Kanda ya Kaskazini ambao kuitia umoja

wao wamehudhuria mafunzo maalumu hivi karibuni. Tunatoa wito kwa makundi mengine ya madereva kuiga mfano huo.

Ili kusajiliwa, dereva anatakiwa kuwa na leseni hai ya udereva, cheti cha mafunzo ya udereva na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA). Dereva anaweza kusajiliwa popote alipo kwa kuwasilisha maombi kupitia anuani ya; <https://rrims.latra.go.tz/login>.

Aidha, LATRA inapenda kuutaarifu umma kuwa baada ya mafanikio ya maboresho ya ratiba za mabasi za kuanza safari saa 11.00 alfajiri, kuanzia tarehe 1 Mei, 2023 Mamlaka itaanza kutoa ratiba za kuanza safari saa 10.00 na 9.00 usiku kwa watoa huduma wenye kuhitaji. Hata hivyo, madereva wa magari haya watapaswa kuwa wamesajiliwa na wanatumia kifaa maalum cha kumtambua dereva anayeendesha gari (i-button).

Imetolewa na:

Johansen J. Kahatano

Kaimu Mkurugenzi Mkuu LATRA

30 Aprili, 2023